**Journal of Kiswahili and Other African Languages**
Vol. 1 No. 2 (2023): ISSN (Online): 2958-4914
DOI: https://doi.org/10.58721/jkal.v1i2.402
*Tafsiri au Uandishi Mpya: Uchambuzi wa Tamthiliya ya Kinjeketile*

# Tafsiri au Uandishi Mpya: Uchambuzi wa Tamthiliya ya Kinjeketile

**Hilda Pembe[1] & Simon Chipanda[2]**
[1]*University of Kansas, United States of America*
[2]*Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, Tanzania*

**Uwasilishaji wa Makala**
*Pokelewa: 2023-09-05*
*Rekebishwa: 2023-12-22*
*Kubalika: 2023-12-29*
*Chapishwa: 2023-12-31*

***Maneno Muhimu***
Tafsiri
Tamthiliya
Mtindo
Ujumbe
Ulinganifu

**Jinsi ya Kurejelea Makala:**
Pembe, H. & Simon, C. (2023). Tafsiri au Uandishi Mpya: Uchambuzi wa Tamthiliya ya Kinjeketile. *Journal of Kiswahili and Other African Languages*, *1*(2), 54-62.

*Copyright* © 2023
CC BY NC SA

**Ikisiri**
Tafsiri hujishughulisha na usafirishaji wa ujumbe ulio katika maandishi kutoka lugha asilia kwenda lugha pokezi ambao hufanywa na mwandishi mwenyewe au mtaalamu mwingine. Makala haya yanachunguza tamthiliya ya Kinjeketile iliyoandikwa kwa Kiswahili kwa mara ya kwanza mwaka 1969 kisha ikatafsiriwa kwa Kiingereza na mwandishi mwenyewe Ebrahimu Hussen kama Kinjeketile mwaka huo huo wa 1969. Kimahususi, makala inachunguza ni kwa namna gani mtafsiri ameweza kuweka usawa wa ujumbe na mtindo baina ya matini asilia na matini pokezi wakati yeye ndiye mwandishi wa tamthiliya hiyo na ameitafsiri mwaka huo huo. Je alitafsiri au aliandika tamthiliya mpya iliyo katika lugha ya Kiingereza? Utafiti umetumia mkabala wa kistahilifu linganishi (correlation qualitative design) kwa kiasi kikubwa japo mkabala wa takwimu umejitokeza kidogo. Data zimekusanywa kwa kutumia mbinu ya upekuzi matini (documentary review). Nadharia ya ulinganifu imetumika katika uchanganuzi wa data kama ilivyojadiliwa na Nida (1964), Catford (1965) na Newmark (1988). Utafiti umebaini kuwa tamthiliya ya Kinjeketile ya Kiingereza ni matini mpya na sio tafsiri kutokana na utofauti wake katika utangulizi, muundo pamoja na idadi na utumizi wa majina ya wahusika.

## Utangulizi

Makala hii inachunguza tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili na kutafsiriwa kwa Kiingereza na mwandishi mwenyewe mwaka huo huo wa 1969 alioandika; Je alitafsiri au aliandika kazi mpya? Sababu ya kuchagua utanzu wa tamthiliya ni kutokana na ugumu wake wa kuitafsiri kwani ni lazima mtafsiri awe mteuzi wa misamiati ambayo itaendana na muktadha wa uigizaji wenye kujenga uhusiano wa wahusika, mandhari na mada. Aidha, uteuzi wa msamiati unafaa kwenda sambamba na ulinganifu wa ujumbe na mtindo baina ya matini asilia (M.A) na matini pokezi (M.P). Ugumu huu wa kutafsiri tamthiliya ndio unaosababisha makala hii kuchunguza ni kwa namna gani Ebrahim Hussen aliweza kuteua misamiati faafu katika usawa wa ujumbe na mtindo baina ya M.A na M.P ya tamthiliya ya *Kinjeketile*. Katika makala hii, uandishi mpya umetafsiriwa kama kitendo cha mtafsiri kutoa ubongoni mwake mawazo mapya na kuyaandika badala ya kuchukua mawazo yaliyo

katika maandishi kutoka lugha moja na kuyaweka katika lugha nyingine kimaandishi. Uandishi mpya hutoa kazi mpya kabisa ambayo haina ulinganifu baina ya M.A na M.P hususani katika mtindo.

Tafsiri ni taaluma inayojishughulisha na mawasiliano ndani ya lugha moja au baina ya lugha mbili au zaidi. Taaluma hii hujihusisha na taaluma nyingine kama vile sheria, elimu, fasihi, isimu na biashara kutokana na kwamba maudhui yanayowasilishwa huhusiana na masuala katika nyanja mbalimbali. Katika taaluma ya fasihi, tafsiri ilikua na kuenea zaidi katika karne ya kumi na nane ambapo waandishi wa kimataifa walitafsiri kazi za fasihi katika lugha zao (Newmark, 1988). Paz (1992) anasema, tafsiri ilileta mwamko na amasa kwa waandishi wa fasihi na kutoa mwelekeo mpya wa fasihi kwa tamaduni lengwa. Maendeleo ya sayansi na teknolojia yamefanya nyanja ya tafsiri na fasihi kukua na kupanuka zaidi.

Kwa mujibu wa Newmark (1988), Mwansoko (1996), Malangwa, 2005 na Pembe (2010), tafsiri za fasihi ikiwemo tamthiliya zina changamoto kubwa kutokana na matumizi ya lugha ya kisanaa, utofauti wa itikadi, dhana, lugha, historia, jiografia, mitazamo na hisia za mwandishi na mtafsiri. Vipengele hivi huweza kusababisha matini kuwa tafsiri finyu, pana au isiyo sahihi na hivyo kutokuwepo kwa ulinganifu baina ya M.A na M.P. Sambamba na changamoto za jumla, ugumu wa kutafsiri tamthiliya pia unatokana na matumizi yake ya lugha ambayo hujikita zaidi katika muktadha na uhusiano kati ya wahusika (Barnstone, 1993; Massoud, 1988). Hivyo mtafsiri wa tamthiliya hulazimika kuelewa muktadha unaozungumziwa na mwandishi wa matini anayotafsiri kabla hajajikita katika mchakato mzima wa tafsiri. Hali hii, humsadia mtafsiri kujua namna ya kuhamisha maana ya maneno kutoka M.A kwenda M.P badala ya kuunda kazi mpya.

Mwandishi anayetafsiri kazi yake mwenyewe huenda akauelewa muktadha aliouandikia kwa urahisi zaidi lakini akashindwa kutoa tafsiri bora ya matini yake mwenyewe na badala yake akatunga kazi mpya. Hii ni kwa sababu kila lugha hujengwa na nduni za kitamaduni, sarufi na jiografia ambazo huweza kujenga muktadha tofauti baina ya M.A na M.P. Ebrahim Hussen ni mwasisi aliyetafsiri kazi yake mwenyewe ambayo ni tamthiliya ya *Kinjeketile* kutoka Kiswahili kwenda Kiingereza. Maswali ya kujiuliza: Je, mwandishi wa tamthiliya ya *Kinjeketile* ametafsiri au ameandika kazi mpya katika lugha ya Kiingereza? Iwapo ameunda kazi mpya, ni vipengele vipi vinavyodhihirisha upya wa kazi hiyo na kama ametafsiri je, kuna usawa wa ujumbe na mtindo baina ya M.A na M.P? Je, mtafsiri anayetafsiri kazi yake mwenyewe na yule anayetafsiri kazi iliyoandikwa na mwingine hutumia vigezo sawa kama vile usawa wa ujumbe, mtindo na muundo wakati wa mchakato wa tafsiri? Iwapo ndivyo, Hivyo basi, makala hii inajaribu kujibu maswali hayo.

**Muhtasari wa Tamthiliya ya *Kinjeketile:*** *Kinjeketile* ni tamthiliya ya kihistoria iliyoandikwa na Ebrahim Hussein mwaka 1969 kwa Kiswahili na kutafsiriwa kwa Kiingereza kama *Kinjeketile* na mwandishi mwenyewe katika mwaka huo huo wa 1969. Tamthiliya ya *Kinjeketile* imejengwa kutokana na historia ya vita vya Maji Maji vya miaka ya 1905-1907 nchini Tanzania kama inavyoelezwa na wanazuoni Illife (1989); Okoth (1992) na Maxon (1994). Ukilinganisha maelezo ya wanazuoni hawa pamoja na maudhui na majina ya wahusika yaliyotumika katika tamthiliya ya *Kinjeketile* unaona uwiano wa karibu sana baina ya tamthiliya hii na historia ya vita vya Maji Maji.

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile*, mwandishi amechora hali halisi ilivyokuwa wakati wa utawala wa Wajerumani. Mwandishi ameonesha jinsi wananchi wa maeneo ya Tanganyika walivyodharauliwa kwa kupigwa viboko, walivyonyang'anywa mashamba yao yenye rutuba, walivyowaua na kuwaoa watoto wao wa kike pamoja na wake zao, walivyofanyishwa kazi katika mashamba ya Wazungu huku wakitozwa kodi katika nchi yao wenyewe. Uchoraji wa maudhui katika tamthiliya ya *Kinjekitile* unawiana na maelezo ya Okoth (1992) anapojadili sababu tatu za kuzuka kwa vita vya Maji Maji

ambazo ni: mpango wa ulimaji wa mazao ya pamba, tabia na mwenendo mbaya wa Wajerumani kwa Watanganyika pamoja na tabia za maakida na askari wa Kiarabu ambao walishirikiana na Wajerumani kuwanyanyasa na kuwaua Watanganyika.

Kutokana na dhuluma na ukandamizaji aliibuka "mtume" Kinjeketile ambaye alionekana kuwa na nguvu za kimuujiza zilizotokana na imani za kidini pamoja na utamaduni zilizosemekana zina uwezo wa kumwondoa Mjerumani. Kinjeketile alitengeneza dawa ya kuwasaidia Watanganyika kumwondoa Mjerumani bila kudhurika kwa kuongozwa na miungu iitwayo *Hongo*. Watanganyika walimwamini Kinjeketile na alifanikiwa kuwaunganisha Watanganyika wote kwa kuwapa imani ya kushinda vita. Kinjeketile alitumia imani za kienyeji, miungu na dawa iliyochanganywa na maji ambayo ilijenga matumaini juu ya umoja, uongozi pamoja na kulindwa. Baada ya muunganiko huo, Watanganyika walishindwa kuvumilia kuendelea na dhuluma na ukandamizaji wa Wajerumani hivyo walikubaliana kuanza vita mara moja pasipo kuwa na ujuzi zaidi wa kumpiga Mjerumani. Walipigana kwa kasi kubwa hadi kufikia kuwa na vita vya msituni. Mwisho wa mapigano hayo, Watanganyika walishindwa kwa kutokuwa na ujuzi wa vita wa kutosha, kutokuwa na umoja na masikilizano baina yao.

Kwa kurejelea usawiri wa mwandishi wa tamthiliya ya *Kinjekitile,* kuna uthibati ya uwiano baina ya jina la Kinjeketile linalojitokeza katika jamii zenye historia ya vita vya Maji Maji (Iliffe, 1989) na lile linalojitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile.* Ithibati hiyo inajitokeza pia kupitia kwa mwandishi mwenyewe katika utangulizi wake pale anaposema 'ningependa kueleza kuwa Kinjeketile ni mtu aliyeishi kweli, aliishi Ngarambe, Tanzania ya Kusini. Hata katika kijitabu kimoja cha historia kinachosimulia vita vya Maji Maji, ametajwa' (Iliffe, 1989).

Kazi hii ilitumia nadharia ya ulinganifu katika uchanganuzi wa data kama ilivyojadiliwa na Eugene Nida (1964) na kuendelezwa na Catford (1965) na Newmark (1988). Nadharia ya ulinganifu iliibuka kutokana na kuwepo kwa tofauti za lugha. Nadharia ya ulinganifu inahusu uwiano au uhusiano wa mtindo na mawazo yanayozungumzwa katika matini asilia (M.A) na yale yanayotafsiriwa katika matini pokezi (M.P) (Nida 1964; Catford, 1965; Newmark, 1988). Uhusiano huo unaweza kujitokeza baina ya lugha mbili au zaidi kwa mfano Kiswahili na Kiingereza au ndani ya lugha moja tu kama vile Kiswahili. Utafiti huu ulijikita katika matini za lugha mbili yaani Kiswahili na Kiingereza. Nida anaendelea kudai kuwa hatuna budi kutumia nadharia ya ulinganifu katika tafsiri kutokana na kwamba mtafsiri anapofanya mchakato wowote wa tafsiri, moja kwa moja huhusisha matini mbili na hivyo hufanya ulinganifu wa matini hizo ama kwa kujua au kwa kutojua. Hali hii ndiyo inayosababisha wataalamu wa tafsiri kudai kuwa nadharia ya ulinganifu hutawala taaluma ya tafsiri. Katika nadharia ya ulinganifu, Nida (1964) ameeleza kwamba ulinganifu hujitokeza kwa kuzingatia utamaduni wa jamii ambayo mtafsiri anaitafsiria. Hii ina maana kwamba mtafsiri hutafsiri kwa kuegemea utamaduni wa hadhira pokezi na hivyo ni wajibu wa mtafsiri kuhakikisha kwamba lugha aliyoitumia inaeleweka vema na kwa urahisi na hadhira lengwa. Hali hii huweza kubainisha dhima mpya ya maneno ambayo yanaweza kuwa na maana tofauti kama yalivyotumika katika M.A kwa lengo la kufanikisha mawasiliano. Mawazo haya ya Nida yanafanana na yale ya Catford (1965) na Newmark (1988) pale wanaposema kwamba ulinganifu hususani wa ujumbe hujitokeza pale mtafsiri anapokuwa huru kutafsiri apendavyo pasipo kufungwa na kanuni za M.A, yaani mtafsiri anatafsiri kwa kuangalia muktadha wa M.P. Nida (1964) anaendelea kusema, nadharia ya ulinganifu pia huweza kujitokeza wakati mtafsiri anajaribu kuweka uhusiano wa karibu iwezekanavyo wa M.A na M.P. Aidha, nadharia ya ulinganifu haimaanishi kwamba mawazo yanayotolewa lazima yawe sawa

kabisa bali humaanisha uhusiano wa mawazo unaweza kukaribiana. Uhusiano huo si lazima ujitokeze katika viwango vyote vilivyomo katika matini husika bali unaweza kujitokeza kwenye baadhi tu ya viwango vilivyoko kwenye matini husika. Hii inadhihirisha kuwa ulinganifu hutegemea aina ya matini, lengo la tafsiri na lugha husika.

Nadharia ya ulinganifu ilifaa katika kazi hii kutokana na kwamba tamthilia ya *Kinjekitile* ya Kiswahili ambayo ni M.A ilihitaji kulingana na tamthilia ya *Kinjekitile* ya Kiingereza katika vipengele vya mtindo, muundo na ujumbe. Ulinganifu huu ndio uliomsaidia mtafiti kutathmini iwapo tamthilia hizi mbili ni uandishi mpya au ni tafsiri. Hivyo basi, kazi hii imetumia mawazo ya Nida, Catford na Newmark kuchunguza namna mtafsiri wa tamthilia ya *Kinjekitile* ameweza ama kutafsiri au kuandika kazi mpya.

**Ukusanyaji wa Data**

Utafiti huu umetumia mkabala wa kistahilifu linganishi ambao hutumika pale suala la utafiti linapojikita katika kulinganisha fenomena (Patton, 1987). Mtafiti amelinganisha M.A na M.P ili kubaini iwapo kuna usawa wa ujumbe na mtindo kwenye tamthiliya teule. Kothari (1992) anaongezea kuwa, mkabala wa kistahilifu linganishi unalenga kutoa data kimaelezo zaidi pasipo kutumia takwimu. Aidha, mbinu ya uchanganuzi wa matini imetumika katika kupata data za uchanganuzi ambapo matini ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili na ile iliyoandikwa kwa Kiingereza zimehusika. Mtafiti amesoma kwa makini matini zote mbili kisha akazilinganisha na kubaini vipengele vinavyofanana na vile vinavyotofautiana ambavyo vilitumika katika uchanganuzi wa data.

**Uwasilishaji na Uchanganuzi**

Katika kufikia lengo la utafiti huu, data zilizokusanywa katika utafiti huu zimegawanywa katika vipengele viwili vikuu ambavyo ni mtindo na usawa wa ujumbe baina ya tamthiliya ya Kinjeketile M.A na M.P. Vipengele hivi ndivyo hasa vinavyoweza kubaini iwapo M.P ni makala mpya au imetafsiriwa.

**Mtindo wa Tamthiliya ya Kinjekitile:** Data zilizokusanywa zimeonyesha kuwa, kuna tofauti ya mtindo baina ya tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili na ile iliyotafsiriwa kwa Kiingereza. Tofauti hizi zimejibainisha katika ruwaza mbili ambazo ni maelezo ya awali kabla ya mchezo wenyewe pamoja na mpangilio wa kazi nzima yaani tamthiliya ya *Kinjeketile*.

**Maelezo ya Awali kabla ya Mchezo wenyewe***:* Maelezo ya awali kabla ya mchezo wenyewe ni mojawapo ya kipengele ambacho kimetumika kubainisha tofauti iliyopo baina ya tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili na ile iliyotafsiriwa kwa Kiingereza. Maelezo ya awali ni muhimu katika kazi za fasihi kwani humsaidia mwandishi kueleza mambo muhimu yaliyomo katika mchezo wake pamoja na muhtasari wa mchezo wenyewe.

Tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili ni matini asili ambayo maelezo ya awali kabla ya mchezo yamegawanyika katika sehemu tatu ambazo ni: kitangulizi, maelezo kwa wachezaji pamoja na maelezo juu ya lugha iliyotumika. Sehemu hizi tatu zimetenganishwa na kufafanuliwa kwa maelezo, kielelezo na michoro. Kwa mfano kitangulizi kimetumia aya kumi na mbili (12) na kuhitimisha kwa kielelezo; maelezo kwa wachezaji yametumia aya kumi na moja (11) ambapo ndani yake kuna sehemu nyingine ndogo iliyopewa jina la "kitendo" na pia kuna mchoro; ilhali maelezo juu ya lugha yametumia aya saba (7). Kiujumla, maelezo ya awali kabla ya mchezo yametumia kurasa tisa (9) na aya thelathini (30).

Tamthiliya ya Kinjeketile iliyoandikwa kwa Kiingereza ni matini pokezi ambayo maelezo ya awali kabla ya mchezo yamegawanywa katika sehemu mbili kuu ambazo ni utangulizi pamoja na ujumbe kwa wachezaji. Sehemu hizi mbili zimefafanuliwa kwa maelezo na kielelezo. Kwa mfano utangulizi umetumia aya kumi na tatu (13) na kuhitimisha kwa kielelezo ilhali sehemu ya ujumbe kwa wachezaji imetumia aya moja tu yenye mistari minne. Kwa ujumla maelezo ya awali kabla ya mchezo yametumia kurasa nne (4) na aya kumi na nne (14).

Ukirejelea maelezo ya awali kabla ya mchezo wenyewe kati ya tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza, unabaini kwamba kuna tofauti katika mtindo wa uwasilishaji. Hii ina maana kwamba, mtafsiri wa tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza hakufuata mpangilio wa maelezo ya awali yaliyomo katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili. Ukiukaji wa mpangilio huo umefanya tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza kuonekana kama matini mpya iliyotungwa na mwandishi na sio tafsiri. Mwansoko (1996) anasema, tafsiri yoyote ile ni lazima iwe na ulinganifu mzuri yaani ulinganifu wa karibu baina ya M.A na M.P la sivyo haitakuwa tafsiri bali kazi mpya.

**Mpangilio wa tamthiliya ya Kinjeketile:** Mpangilio ni miongoni mwa vipengele vinavyodhihirisha tofauti kati ya tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza. Tofauti hii imejitokeza katika vipengele vifuatavyo: utokeaji wa ukimya, upangaji wa sehemu za mchezo na matumizi na upangaji wa majina ya wahusika ndani ya tamthiliya.

**Utokeaji wa Kimya:** Kipengele cha utokeaji wa ukimya kimetofautiana baina ya tamthiliya ya *Kinjeketile* iliyoandikwa kwa Kiswahili na ile iliyoandikwa kwa Kiingereza kama ifuatavyo:

***Data A.***
**M.A:** **Bi Kitunda**: Kweli mimi simuoni. Lakini nanna gani yeye anaweza kukaa ndani bila kwenda shambani?

**Bi Kinjeketile:** Sijui, pengine amekwenda. Mimi sendi kuntazamatazama

**Bi Kitunda:** Siku moja nikankuta ntoni peke yake. Mimi nilikwenda kalibu akuniona. Alikuwa anafata nto unakotokea. Anatazama maji kama hajayaona.

**Bi Kinjeketile:** Kabadilika sana. Analosema mimi silisikii. Aya kwa heli

**Bi Kitunda:** Kwa heli. (Wanaachana. Kimya. Bi Kitunda na mtoto wake wamebaki peke yao. Wanatazama moshi unaotoka …) (uk. 2).

**M.P:** **Bibi Kitunda:** Yes, I don't see him very often these days. But how can he stay in and not go to the plantation?

**Bibi Kinjeketile:** I don't know…. Perhaps he goes… I don't go peering into his affairs too closely.

(Pause)

**Bibi Kitunda:** Some time ago, I met him at the river alone. I went near him-very near, but he didn't see me. He was looking at the water, very strangely; as if he had never seen it before.

**Bibi Kinjeketile:** He's changed a lot. I don't understand what he says any more. Well, goodbye (uk. 2).

Ulinganishi wa M.A na M.P katika data A unabaini kwamba kuna uingizaji wa neno kimya katika M.P ambalo linaleta utofauti baina ya M.A na M.P. Uingizaji wa maneno katika tafsiri hukubalika pale tu inapobidi yaani neno lisipoingizwa huweza kuathiri maana ya sentensi iliyokusudiwa. Katika data A uingizaji wa neno kimya si wa lazima katika M.P kwani hata ukilitoa hakuna athari yoyote katika ujumbe. Kwa mujibu wa Newmark (1988), mtafsiri wa kazi yoyote huwajibika kulinda mtindo wa M.A awezavyo ili kukidhi kanuni za tafsiri na sio kuunda kazi mpya. Utofauti wa utokeaji wa neno kimya umejitokeza pia katika ukurasa 7 wa M.A, na kurasa 13, 52 na 53 wa M.P. Kuingizwa kwa

neno kimya katika M.P kunaifanya matini hiyo itofautiane na mtindo wa M.A na hivyo kuonekana kama matini mpya na wala si tafsiri.

**Upangaji wa Sehemu za Mchezo:** Ulinganishi wa tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza unabaini kuwa mpangalio wa sehemu za mchezo umejitokeza sawa kwenye matini zote mbili kwani matini zote zina sehemu nne. Pamoja na usawa wa utokeaji wa sehemu katika tamthiliya ya *Kinjeketile* lakini kuna utofauti wa upangaji wa maonyesho ndani ya sehemu hususani katika sehemu ya kwanza. Sehemu ya kwanza ya tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili ina maonyesho matatu (3) ilhali katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza inaonesha maonyesho mawili (2). Utofauti huu wa maonyesho ndani ya sehemu moja unadhihirisha kwamba mtafsiri ambaye ndiye mwandishi wa tamthiliya ya *Kinjeketile* hakutafsiri bali aliyaweka matukio yake katika lugha ya Kiingereza na hivyo kusababisha tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza kuonekana kama ni kazi mpya na sio tafsiri.

**Matumizi na Upangaji wa majina ya wahusika ndani ya tamthiliya:** Matumizi na upangaji wa majina ya wahusika ndani ya tamthiliya ya *Kinjeketile* umetofautiana baina ya matini asilia na matini pokezi. Kuna baadhi ya wahusika ambao wamejitokeza katika Matini Asilia ila hawajajitokeza katika Matini Pokezi. Kwa mfano, villagers, Kitunda's son, Men of the people's army, na Daudi. Wahusika hawa wote hawajajitokeza katika Matini Asilia. Hali hii inaonyesha tofauti baina ya Matini Asilia na Matini Pokezi. Sambamba na hilo, mwandishi pia ametumia majina ya jumla badala ya majina maalumu kama yalivyojitokeza katika Matini Pokezi. Kwa mfano, mwandishi ametumia wahusika kama wazee, wanawake na askari lakini katika matini pokezi mtafsiri ametumia wahusika hawa kimaalumu kama vile mzee wa kwanza, mzee wa pili na mzee wa tatu; mwanamke wa kwanza, mwanamke wa pili; pamoja na askari wa kwanza na askari wa pili. Hali hii inaonyesha utofauti wa matumizi na upangaji wa wahusika na hivyo kuhitimisha kuwa mtafsiri hakutafsiri bali aliandika matini mpya.

**Usawa wa Ujumbe**

Katika kuchambua usawa wa ujumbe, tulijikita katika *matumizi ya alama za uakifishaji.* Ogechi (2002) anasema alama za uakifishaji ni mojawazo ya njia inayofanikisha mawasiliano na iwapo zitatumika visivyo basi zinaweza kuleta utata katika ujumbe unaowasilishwa. Matumizi haya ya alama za uakifishaji yanasisitizwa hata kwa mtafsiri yeyote anapokuwa katika mchakato wa tafsiri. Reiss (2000) anasema pamoja na utofauti wa lugha, historia, mazingira na utamaduni kuathiri tafsiri, lazima mtafsiri awe makini katika matumizi ya alama za uakifishaji kwani wakati mwingine zinaweza kuleta utofauti wa maana baina ya M.A na M.P na hivyo kusababisha ujenzi wa kazi mpya.

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza,kuna tofauti katika matumizi ya alama za uakifishaji kama ifuatavyo:

*(a) Matumizi ya alama ya kiulizo (?) na mshangao (!):*
**MA: Mnyapala:** Lakini siku mbili kidogo? Fikili, siku mbili bila kazi (uk. 8)
**MP: Mnyapala:** But think, two days! Two days with no work (uk. 9)
*(b) Matumizi ya dukuduku (…) na kistari (-)*

**MA: Mnyapala:** Bwana askali-hata bwana Thabiti kakubali-bwana askali, kama nilivyokuwa nikisema, kuwa amesema unaweza kupumzika kesho (uk. 8)
**MP: Mnyapala:** Bwana Askari, and even Bwana Akida-Thabiti, have agree to this…. Yes-as I was saying… Bwana Askari says you can rest tomorrow…. (uk. 9)

Mifano hii miwili yaani (a) na (b) tofauti inadhihirika katika matumizi ya alama za uakifishaji. Katika mfano (a) M.A imetumia alama ya kiulizo ilhali M.P imetumia alama ya mshangao. Tofauti ya matumizi ya alama hizi unajenga maana tofauti katika matini hizi mbili na hivyo kusababisha kuwepo na utofauti wa M.A na M.P. Katika mfano (b), M.P imetumia alama za dukuduku ambazo hazipo katika M.A. Matumizi haya ya dukuduku yamejitokeza kwa wingi katika M.P kwenye ukurasa wa 2, 9, 12, 27, 30, 35, 37 na 43.

Pia kuna matumizi ya alama ya kistari ambayo yanaonyesha tofauti baina ya M.A na M.P. Katika M.A mwandishi ametumia kistari katika neno "askali-hata" na neno "kakubali-bwana askali" ukirejea M.P mtafsiri hakutumia alama ya kistari katika maneno hayo na badala yake ametumia kistari katika maneno mengine kama vile "akida-Thabiti" na "Yes-as".

Kwa kurejelea data za M.A na M.P katika tamthiliya ya *Kinjeketile,* unadhihirisha kuwa kuna tofauti za utumiaji wa alama za uakifishaji ambazo zimefanya matini hizi mbili kuonekana kama ni matini mbili tofauti. Kwa kujibu wa Ogechi 2002, alama za uakifishaji zinapotumika tofauti katika sentensi zinasababisha maana tofauti ya sentensi. Kwa mfano matumizi ya alama ya kiulizo na alama ya mshangao katika M.A "Lakini siku mbili kidogo?" na M.P "But think, two days!". Sentensi hizi mbili zinaleta maana tofauti kabisa kutokana na kutumia alama tofauti za uakifishaji.

**Matumizi ya Majina ya Wahusika***:* Wahusika ni viumbe wanaoweza kuwa binadamu au wanyama wenye kuteuliwa au kusukwa kwa namna fulani kwa lengo la kuwasilisha sifa fulani fulani za ubinadamu (Wamitila 2006; Njogu & Chimerah, 2008). Katika kazi ya fasihi wahusika hutofautiana kutokana na lengo la msanii, aina ya kazi ya fasihi na uwezo wa kisanaa alionao mwandishi katika kuteua na kujenga wahusika katika fasihi.

Katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili, mwandishi ameorodhesha majina ya wahusika 17 mwanzoni mwa kitabu lakini katika kuelezea matukio yake ametumia majina ya wahusika 38 ilhali katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza, mtafsiri ameorodhesha majina ya wahusika 30 mwanzoni mwa kitabu lakini katika kuelezea matukio yake ametumia majina ya wahusika 32. Majina ambayo yametumika katika M.A na yale hayamo katika M.P ni yafuatayo: Mabibi, Mzaramo, Bwana wa IV, Mjumbe, Wengine na Afisa. Sambamba na hilo, mhusika Mjumbe na mhusika Mjumbe wa Wazaramo wametumika tofauti katika M.P na M.A. M.P imetumia mhusika Mjumbe na mhusika Mjumbe wa wazaramo ni mhusika mmoja wakati katika M.A mhusika mjumbe na mhusika Mjumbe wa Wazaramo hawa ni wahusika wawili tofauti. Vilevile, M.P imetumia jina la mhusika Afisa wa Kijerumani kwenye jina la Afisa na kufanya ni mhusika mmoja ilhali M.A imetumia majina ya wahusika wote wawili yaani Afisa wa Kijerumani na Afisa kama majina ya wahusika wawili tofauti. Ujumuishaji wa majina ya wahusika katika M.P ndio imesababisha utofauti wa majina ya wahusika baina ya M.A na M.P na hivyo kuonekana kama ni kazi mbili tofauti.

Pia, M.P imedondosha wahusika ambao ni: Mabibi, Bwana wa IV, Mjumbe na Wengine na kufanya mawazo yao yachukuliwe na wahusika wengine. Udondoshaji huu umesababisha mpishano wa idadi ya wahusika baina ya M.A na M.P. Tofauti hii ya majina ya wahusika inachangia katika kuonyesha kuwa M.A na M.P ni tungo mbili tofauti. Kutokana na utofauti huu wa idadi ya majina ya wahusika pamoja na matumizi yake inadhihirisha kwamba tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza siyo tafsiri bali ni matini mpya inayojitegemea.

Mbali na udondoshaji wa majina ya wahusika, kuna utofauti wa upangaji wa majina ya wahusika ambao umejitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza kama ifuatavyo:

**MA:** **Mtu III:** Hata mimi nasema ivyo ivyo, huyu ni Hongo

**Kizee II:** Hongo hachukui watu. Hongo anapanda kichwani
**Kizee:** Aha! Maneno gani…
**Kitunda**: Hebu tusikilizane, jamani. Mimi nasema tuanze kutafuta hivi sasa

**MP:** **First Old Man:** I said so myself. This is clearly Hongo's doing.
**Second Old Man:** Hongo does not take people away. He merely possesses them.
**First Old Man:** Nonsense. What rubbish….
**Kitunda:** Please let us listen to one another. For my part, I suggest that we start looking now.

Katika MA mwandishi ametumia mhusika Mtu III ilhali katika M.P mtafsiri ametumia mhusika Mtu wa Kwanza. Vilevile katika MA mwandishi ametumia jina la mhusika Kizee ilhali katika M.P mtafsiri ametumia Kizee wa Kwanza. Sambamba na utumiaji huo inaonesha kwamba mtafsiri ameshindwa kutofautisha neno *kizee* na *mtu* na hivyo kuleta utata ambao umejenga utofauti wa matini hizo mbili. Kwa kuangalia maelezo haya inaonekana kwamba kuna utofauti mkubwa baina ya M.A na M.P na hivyo kudhihirisha kwamba tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza ni matini mpya na sio tafsiri.

**Hitimisho**

Tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza ni matini mpya na sio tafsiri kutokana na utofauti wake katika vipengele mbalimbali kama vile utangulizi, muundo pamoja na idadi na majina ya wahusika waliotumiwa. Katika utangulizi kuna baadhi ya sehemu ambazo hazijatafsiriwa kabisa bali zimeingizwa katika M.P. Kutotafsiri kwa sehemu hizo kumeifanya M.P kuonekana kama haina uhusiano wowote na M.A. Kipengele kingine kinachoonyesha upya wa tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza ni muundo wake. Utofauti wa vipengele vya muundo kama vile utokeaji wa ukimya, mpangilio wa sehemu mbalimbali na matumizi ya alama za uakifishaji uliojitokeza katika tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiingereza umeifanya matini hii kuonekana kuwa ni matini mpya na wala sio tafsiri kwani kumekuwa na ulinganifu wa mbali sana na ile tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili. Vilevile tofauti katika majina ya wahusika yaliyotumiwa baina ya tamthiliya ya *Kinjeketile* ya Kiswahili na ile ya Kiingereza umeonyesha wazi kuwa mwandishi hakuitafsiri tamthilia ya Kiswahili kwa Kiingereza bali ameandika tu tamthiliya mpya kwa Kiingereza. Kutokana na tofauti katika vipengele mbalimbali katika M.A na M.P, makala hii inahitimisha kuwa Ebrahim Hussein aliandika tamthiliya mbili tofauti yaani tamthiliya ya kwanza ni Kinjeketile kwa Kiswahili na ya pili ni Kinjeketile kwa Kiingereza.

**Marejeleo**

Barnstone, N. (1993). *The Poetics of Translation: History, Theory, Practice*, Kingsley Trust Association Publication Fund
Catford, J. C. (1993). *A Linguistic Theory of Translation: An Essay in Applied Linguistics*. Oxford University Press.
Hussen, E. N (1969). *Kinjeketile.* (Toleo la Kiswahili). Oxford University Press.
Hussen, E. N (1969). Kinjeketile. (Toleo la Kiingereza). Oxford University Press.
Ilife, J. (1989). *A Modern History of Tanganyika*. Cambridge University Press.
Malangwa, P. S. (2005). Problems of Translating Literary Works: The Case of Julius Kambarage Nyerere's Translation of the Play Mabepari wa Venisi[Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam Haijachapishwa]
Massoud, M. (1988), *Translate to Communicate: A Guide for translation*. David: Cook Foundation.
Maxon, M. R. (1994). *East Africa: An Introduction History*. E. A. E. P
Msokile, M. (1992). *Kunga za Fasihi na Lugha*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
Mwansoko, H. J. M. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri: Nadharia na Mbinu*. TUKI.

Newmark, P. (1988). *Approaches to Translation, Singapore*. Prentice Hall International Ltd.
Njogu, K. & Chimerah, R. (2008). *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na Mbinu*. The Jomo Kenyatta.
Okoth, A. (1992). *A History of Africa*. 1855-1914. E. A. E. P
Ogechi, N. O (2002). *Mbinu za Mawasiliano kwa Kiswahili*. Moi University Press.
Paz, O. (1992), "Translation, Literature and Letter" in R. Schulte and J. Biguenet (Eds), Theories of Translation. University of Chicago Press. pp. 68-69
Pembe, H. (2010). The Challenges of Translating Poetic Texts: The Case of Paul Sozigwa's Wimbo wa Lawino [Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Haijachapishwa]
Pym, A. (2010). *Exploring Translation Theories*. Routledge.
Reiss, K. (2000). *Translation Criticism-The Potentials and limitations*. America Bible Society
Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi: Mfululizo wa Lugha na Fasihi Kitabu cha Kwanza*. KAUTTU.
Wamitila, K. W. (2006). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.